

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KYELA

SHULE YA SEKONDARI KYELA,

S.L.P 18,

**KYELA – MBEYA**

20/05/2021.

SIMU NO. **1. 0767/0784 – 465132**

**2. 0753-468391**

UNAPOJIBU TAFADHALI TAJA

KUMB. NA. HWK/KYLSS./JINST.24/VOL1./12

MZAZI / MLEZI WA .....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYELA KIDATO CHA TANO ..... (JOINING INSTRUCTIONS)**

**a) UTANGULIZI:**

Ninayofuraha kukujulisha kuwa mwanao ..... amechaguliwa kujiunga na shule ya Sekondari Kyela kuanza kidato cha Tano (V) katika tahasusi (combination) ya ..... (HGK, HGL, HKL, PCB, PCM na CBG). Natumia fursa hii kumpongeza mwanao kwa mafanikio hayo, **Hongera sana.**

Shule itafunguliwa rasmi tarehe **03 /07/2021** na mwanafunzi anatakiwa kufika siku hiyo bila kukosa.

Ili kujiunga na shule hii mwanafunzi anatakiwa awe amekamilisha mambo yafuatayo:-

- i. Ajaze fomu ya kukubali kujiunga na shule kwa usahihi akishirikiana na Mzazi/Mlezi wake. (kiambatanisho 'A')
- ii. Ajaze taarifa binafsi ya mwanafunzi kwa usahihi na ukamilifu katika fomu (kiambatanisho 'B')
- iii. Mwanafunzi apimwe afya yake Hospitalini na kujaza taarifa zake kiafya katika fomu ya 'Request for Medical examination' (kiambatanisho C).
- iv. Mwanafunzi akamilishe maagizo yote yaliyoandikwa katika fomu ya mahitaji ya lazima ya shule kama ilivyoainishwa katika maagizo ya kujiunga na shule hii.

Baada ya kukamilisha maagizo yote hapo juu, hakikisha kuwa mwanafunzi anakuja na fomu hizo kuripoti shuleni siku ya kwanza.

Kitendo cha kuchelewa kuripoti shuleni kinaweza kusababisha mwanafunzi kukosa nafasi ya kujiunga na shule hii na nafasi yake kujazwa na mwanafunzi wa akiba (second selection).

Endapo mwanafunzi aliyechaguliwa ameshindwa kujiunga na shule hii atatakiwa kutoa taarifa ya maandishi mapema kabla ya siku 30 tangu shule kufunguliwa kwa Mkuu wa Shule kwa kutumia anuani ifuatayo:-

MKUU WA SHULE,  
SHULE YA SEKONDARI KYELA,  
S.L.P18, KYELA. **Namba ya Simu. 0784/0767-465132**

## **b) MAHALI SHULE ILIPO**

Shule iko Mkoani Mbeya Wilayani Kyela km 1.5 kutoka makao makuu ya Wilaya. Unaweza kutembea kwa mguu au pikipiki nauli ni shilingi elfu moja (1000/=).

## **2. Mambo muhimu ya kuzingatia**

### **2.1 Sare**

- a) Suruali rangi ya mkapa blue mbili (2) zenye rinda na zisiwe modo. (Waweza kupata shuleni)
- b) Mashati ya mikono mirefu meupe mawili (2).
- c) Track suit moja rangi ya zambarau (Mbeya city), bukta Na T-shirt yake moja rangi nyekundu na michirizi nyeupe.
- d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
- e) Soksi rangi ya kaki za kutosha.
- f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.
- g) Sweta rangi ya blue.
- h) Nguo za kushindia (shamba dress) suruali khaki mbili (2) na T-shirt mbili form six rangi ya zambarau zenye nembo ya shule. (Tsh.15,000/= moja) zinapatikana shuleni.
- i) Tai mbili (2) rangi ya mkapa blue ndefu.
- j) Lab coat kwa wanafunzi wa sayansi.
- k) Mwanafunzi anatakiwa awe na bima ya afya
- l) **Result slip** (original) na **cheti cha kuzaliwa** au cheti cha ubatizo au kadi ya kliniki

NB:

- ❖ Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za ziada/ kuvaa au kupatikana na mavazi ya aina nyingine yoyote ya kiraia nje na sare au shamba dress au track suit kama ilivyoainishwa hapo juu.

Atakayepatikana na mavazi tofauti na hapo juu akiwa amevaa shuleni na au amezitunza Bwenini atapewa adhabu kali na kuziteketeza nguo hizo yeye mwenyewe

## 2.2 Ada na michango ya shule

(a) Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi 70,000/= kwa mwanafunzi wa bweni. Unaweza kulipa kiasi cha shilingi 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule **kupitia Benki ya NMB Account No. Na 60901200046 KYELA SEKONDARI ( tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip)**

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-

- i) Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
  - ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho.
  - iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
  - iv) Shilingi 30,000/ kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
  - v) Shilingi 5000 huduma ya kwanza.
  - vi) Shilingi 20,000/= mitihani yakujipima.
  - vii) Fedha ya tahadhari 5000/=.
- Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti ya shule Na 60901200046 katika Benki ya NMB. (tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip) LETE BPS SIKU UNAYORIPOTI.

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:-

- i) Ream ya karatasi 1, graph paper 2 na file 1 la kaki
- ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika
- iii) Unashauriwa kuleta daftari kubwa lenye kurasa nyingi kulingana na tahasusi yako.
- vi) Dissecting kit kwa mwanafunzi wa biolojia (original).
- v) Stop watch kwa tahasusi za sayansi.
- vi) Scientific calculator
- vii) Mashuka blue bahari pea 2, foronya 1, chandarua 1 ya pembe nne nyeupe.
- viii) Kolabo 1, kijiko na kikombe.
- ix) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko.
- x) Vifaa vya usafi binafsi (Yebo pair 1, sabuni ya kuogea na kufulia na taulo.
- xi) Fagio laini 1, fagio gumu 1, squeezer 1, mopa 1 na sabuni ya unga kilo mbili.

### **3. MAKOSA YATAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

- i) Wizi.
- ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/ utoro.
- iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.
- iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
- v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kupigana na mwalimu au mtu yeyote yule.
- vi) Kufuga ndevu
- vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
- viii) Uvutaji wa sigara
- ix) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja
- x) Kusababisha ujauzito
- xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
- xii) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
- xiii) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- xiv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
- xv) Kudharau Bendera ya Taifa
- xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- xvii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi mfano madawati, kuchora kuta nk.

#### **4. Viambatisho na fomu Muhimu**

- a) Fomu ya ukaguzi wa Afya (medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya serikali.
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria. Kanuni kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
- d) Picha nne (4) za Wazazi na Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

.....  
MWAIHOJO A.J

MKUU WA SHULE.

**Kiambata A**  
**FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYELA.**

**A. Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi ..... Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha kwanza/tano ..... Katika shule ya Sekondari ya Kyela na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni .....  
.....  
.....  
.....

**B. Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi ..... ninakubali mtoto wangu .....  
Kuchukua nafasi kuingia Kyela shule ya sekondari kidato cha .....  
Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule Kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.  
Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni:-  
.....  
.....  
.....  
.....

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Sahihi..... Tarehe .....

Kiambata "B"

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina lako kamili lilivyotumika kidato cha nne.....  
Dini yako/dhehebu .....
2. Jina kamili la baba mzazi/mlezi .....
- Kazi yake .....
- Anwani kamili ya baba mzazi/mlezi .....
- Na. yake ya simu ya mkononi .....
- Na. yake ya simu ya mezani .....
- Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa ..... Wilaya .....
- Tarafa ..... Kata .....Kijiji/Mtaa.....
3. Jina kamili la mama mzazi/mlezi .....
- Kazi yake .....
- Anwani kamili ya mama mzazi/mlezi .....
- Na. yake ya simu ya mkononi .....
- Na. yake ya simu mezani .....
  
- Mahali anakoishi mama mzazi/mlezi: Mkoa ..... Wilaya .....
- Tarafa .....Kata ..... Kijiji /Mtaa.....
4. Majina ya watu wanne wanaoruhusiwa kumtembelea/kumchukua mtoto wako

<b>Na.</b>	<b>Jina lake</b>	<b>Uhusiano</b>	<b>Mahali anakoishi</b>	<b>Anwani na namba yake ya simu</b>
01				
02				
03				
04				

**5. shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne**

<b>Na</b>	<b>Jina la shule</b>	<b>Darasa /Kidato</b>	<b>Kuanzia mwaka hadi mwaka</b>	<b>Mkoa</b>	<b>Wilaya</b>	<b>Kijiji/Kata</b>
<b>01</b>						
<b>02</b>						
<b>03</b>						
<b>04</b>						

Namba yangu ya mtihani wa kidato cha nne .....

**6. Matokeo yangu ya mtihani wa kidato cha nne**

<b>Na.</b>	<b>Somo</b>	<b>Daraja</b>	<b>Na.</b>	<b>Somo</b>	<b>Daraja</b>
<b>01</b>					
<b>02</b>					
<b>03</b>					
<b>04</b>					
<b>05</b>					
<b>06</b>					
<b>07</b>					
<b>08</b>					
<b>09</b>					
<b>10</b>					

Nilipata divisheni ..... pointi .....

7. Tarehe niliyoripoti hapa kyela Sekondari ni .....

Masomo nitakayosoma ni:-

1. .... 2. .... 3. ....  
4. .... 5. .... 6. ....

Matarajio yangu baada ya kuhitimu masomo yangu mfano kuwa Daktari, Mwanasheria n.k

1. ....  
2. ....  
3. ....

Hapa shuleni ningependa niujiunge na

1. Michezo (i) .....(ii) .....(iii).....  
2. Kikundi cha utamaduni wa .....  
3. Mradi wa .....

8. Taja kipaji maalumu ulichonacho na ungependa kukiendeleza:-

.....  
.....  
.....  
.....  
.....  
.....

Kiambata "C

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA  
PRESIDENT'S OFFICE  
REGIONAL ADMINISTRATIVE AND LOCAL GOVERNMENTS  
KYELA DISTRICT COUNCIL**

KYELA SECONDARY SCHOOL,  
P.O BOX 18,  
**KYELA**

**DATE.....**

**DISTRICT MEDICAL OFFICER  
P.O.BOX .....**

.....

**Dear Sir/Madam.**

**Re : A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine Mr./Miss ..... as to his/her physical and mental fitness for admission as a Form Five Student at Kyela secondary school in the year 2021.

Yours sincerely,

.....  
**A. J. MWAIHOJO  
HEAD OF SCHOOL**

---

The Headmaster,

I have examine Mr./Miss .....as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1. Vision with/without glasses. Right ..... left .....
2. Blood pressure ..... Haemoglobin .....
3. Hearing .....
4. Urine (a) Albumen ..... (b) Sugar .....
5. (a) Venereal diseases .....(b) Bilharzia .....
6. Pregnancy .....
7. Neurosis .....
8. Is there any abnormality of:-  
(a) The heart ..... (b) Lungs .....
- (c) The spleen .....

9. Are there any serious diseases e.g. leprosy, epilepsy, asthma, diabetes etc.

Any comments .....

Date: .....

.....

Signature of Medical Officer

Station:.....

Designation.....



Kiambata "D"

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA.....**

OFISI YA MKUU WA WILAYA,  
WILAYA YA .....,  
S.L.P .....,  
TAREHE .....

MKUU WA SHULE,  
SHULE YA SEKONDARI KYELA,  
S.L.P 18,  
**KYELA  
MBEYA**

**YAH: UTHIBITISHO WA URAIA.**

Nathibitisha kuwa ..... (jina kamili la mwanafunzi) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa /kwa kuandikishwa.

Baba yake (jina kamili) .....  
Amezaliwa katika Mkoa wa ..... Wilaya ya .....  
Tarafa ya ..... Kata ya .....  
Mama yake (jina kamili) .....  
Amezaliwa katika Kata ya ..... Wilaya ya .....  
Hapa nchini.

.....  
**MKUU WA WILAYA**

**NB: Kila mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu. Ikishajazwa irudishwe kwa Mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni.**